

TUMSIFU MUNGU.

L.G.S

♩ = 90



1. Kwa a ji li ya ndu gu ju a te na na ye da da mwe zi



1. njo 'ni vi u mbe pa mo ja tu m si fu ni Mwenye zi.

2. Aliumba vitu vyote,
Mbinguni na duniani,
Vingine kavipa pumzi,
Ili vimumikie.

3. Ndege samaki kaumba
Malaika kawaumba,
Watu wanyama mimea,
Apaswa kuabudiwa.

4. Watu walipokosea,
Neno akatwaa mwili,
Akafa msalabani,
Kututoa utumwani.


5. Roho akatushukia,
Paji zake kututia,
Tuweze kutumikia,
Vema bila kukosea.

6. Baba yu ndani ya Mwana,
Roho yu pamoja naye,
Nasi twaabudu mmoja,
Nafsi zake twazijua.

Kiitikio

5

Si fa



Si fa kwa ke Mu ngu Ba ba pi a zi we na kwa Mwa na


7

na kwa



na kwa Ro ho Mta ka ti fu hu yu hu yu ni Mu ngu m mo ja

9



mi le le.